



**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**  
**OFISI YA RAIS - KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA**  
**BORA**

S.L.P. 3356/772  
MAZIZINI ZANZIBAR- TANZANIA

SIMU : 024 2230034  
FAX : 024 2230027

**CAB.40/158/01/17**

**07/09/2018**

**MAKATIBU WAKUU WA WIZARA ZA SMZ**  
**ZANZIBAR.**

**WAKUU WA MIKOA**  
**ZANZIBAR.**

**WAKUU WA IDARA MAALUM ZA SMZ**  
**ZANZIBAR.**

**WAKUU WA MASHIRIKA, MAMLAKA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA**  
**ZANZIBAR.**

**MAAFISA WADHAMINI,**  
**PEMBA.**

**KUH: KUENZISHWA KWA SIKU YA UTUMISHI WA UMMA ZANZIBAR.**

Kwa heshima naomba uhusike na mada ya hapo juu.

Napenda kukuarifu kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeridhia kuanzishwa kwa siku ya Utumishi wa Umma nchini kwa lengo la kuipa hadhi sekta ya Utumishi wa Umma, kuimarisha Huduma kwa jamii na kuwawezesha Watumishi wa Umma kutambua Dira, Dhima, Malengo, Programu, Mikakati, Mafanikio na Changamoto zinazoikabili Tasnia ya Utumishi wa Umma Zanzibar.

Kwa kawaida, maadhimisho ya siku ya Utumishi wa Umma ni muendelezo wa makubaliano ya Mkutano Mkuu wa nne wa Mawaziri wenye dhamana ya Utumishi wa Umma. Mkutano ulioamua kuhusu uadhimishaji wa siku ya Utumishi wa Umma ambayo itakuwa ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Utawala Bora na Utumishi wa Umma chini ya Umoja wa Africa.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeruhusu kuandhimishwa siku ya Utumishi wa Umma Zanzibar kila ifikapo tarehe 17, Julai ya kila mwaka na kuadhimisha kilele cha siku hiyo tarehe 23, Juni ya kila mwaka. Katika kufanikisha maadhimisho hayo, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora, itakuwa ndio msimamizi na mratibu mkuu wa Maadhimisho hayo, maadhimisho ambayo yatajumuisha mambo mbali mbali yakiwemo yafuatayo:-


- I. **Kuanzishwa kwa Makongamano:** yenye lengo la kujadili masuala mbali mbali yanayohusu Utumishi wa Umma, pamoja na kutoa fursa kwa Watumishi, Wananchi na Wadau mbali mbali kuelezea changamoto mbalimbali zinazowakabili katika kutoa na kupata huduma.
- II. **Maonyesho:** Kutakuwa na maonyesho ya Kitaifa yatakayofanyika kuonyesha huduma mbali mbali zinazotolewa na Taasisi za Umma kwa kuzingatia kauli mbiu ya Maadhimisho hayo.
- III. **Tunzo na Sherehe:** Katika kujali utendaji kazi na utoaji wa Huduma bora kwa Jamii, Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma itaandaa zawadi Maalum kwa Taasisi itakayoongoza kutoa huduma bora kwa Jamii.

Katika kutekeleza maadhimisho haya, Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinatakiwa kushirika kikamilifu katika Maadhimisho ya Siku ya Utumishi wa Umma Zanzibar pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya wiki ya Utumishi wa Umma Zanzibar kwa kila mwaka.

Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma itazitaarifu rasmi Wizara, Mashirika, Mamlaka na Taasisi zinazojitegemea za SMZ kuhusu maadalizi ya uanzishwaji wa maadhimisho hayo kila mwaka kabla ya tarehe ya maadhimisho hayo kufika.

Naomba kuwasilisha kwa hatua.

Wako mtiifu.

  
**YAKOUT H. YAKOUT.**  
**KATIBU MKUU,**  
**(OR) KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UATWALA BORA,**  
**ZANZIBAR.**

**NAKALA.**

Katibu wa Baraza la Mapinduzi,  
na Katibu Mkuu Kiongozi,  
**Zanzibar.**

Mheshimiwa Waziri wa Nchi,  
(OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora,  
**Zanzibar.**

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi  
(OR)- Katiba Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora  
**Zanzibar.**